MUONGOZO WA USAHIHISHAJI

1. **SEHEMU A** ( ALAMA 16)

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| I | Ii | iii | iv | v | Vi | vii | Viii | ix | x |
| D | C | E | A | B | C | A | D | B | E |

2.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| i | ii | iii | Iv | v | Vi |
| F | E | G | D | C | B |

**SEHEMU B** ( ALAMA 54)

3. (A) Mwanafunzi aoneshe namna viambishi awali vinavyoweza kuonesha viambishi ngeli na idadi katika nomino kwa mifano thabiti (Alama 1@ hoja)

i. Huonesha idadi ya umoja na wingi katika nomino
Mfano M-guu Mi-guu
Ji-cho Ma-cho
M-refu Wa-refu
Ki-ti Vi-ti

ii Huonesha ukubwa wa nomino

Mfano Ji-tu Ma-jitu

Ju-mba Ma-jumba

Ji-ti Ma-jiti

iii Huonesha udogo wa nomino

Mfano Ki-toto Wa-toto

Ki-vulana Vi-vulana

Ki-sichana Vi-sichana

(B) Mwanafunzi aoneshe miundo miundo minne(4) ya nahau

i. Muundo wa kitenzi na nomino( T+N) Mfano Vunja mbavu
ii. Muundo wa nomino na kivumishi (N+V) Mfano Ndege mbaya
iii. Muundo wa kitenzi na kielezi(T+E) Mfano Yatakutokea puani
iv. Muundo wa nomino na nomino (N+N) Mfano Domo zege

(C) Mwanafunzi na aoneshe maana za dhana zifuatazo kwa kutoa mifano thabiti

i. Kiambishi awali cha kauli ya kujitendea ni kiambishi kinachoandikwa kabla ya mzizi wa kitenzi ili kuonesha dhima ya kujirejelea
Mfano Nimejisomea **'ji'** kuonesha kauli ya kujirejelea
Anajikata '**ji**' kuonesha kauli ya kujirejelea
Walijikata **'ji'** kuonesha kauli ya kujirejelea

ii. Kiambishi awali kipatanishi ni kiambishi kilichopo katika kitenzi au kivumishi ambacho huleta upatanisho baina ya nomino, kivumishi au kitenzi kwa kuzingatia ngeli za nomino husika

Mfano Kiambishi awali cha nafsi ya kwanza Ninasoma kitabu

Kiambishi awali nafsi ya pili Unasoma vizuri

4. (A) Mwanafunzi na aoneshe chanzo au njia zinazopelekea utokeaji wa Simo/ misimu katika jamii (Alama 1@ hoja)

(i) Njia ya kutohoa kutoka katika lugha ya kigeni Mfano neno Fegi
(ii) Njia ya kutumia sitiari Mfano Amevaa chupa
(iii) Njia ya kutumia tanakali sauti Mfano Mataputapu
(iv) Njia ya kubadili maana ya msingi Mfano Hassani amemfia sana

(B) Mwanafunzi na aeleze athari tano(5) zitokanazo na matumizi mabaya ya Simo/ misimu

i .Simo huaribu lugha kwani si lugha sanifu
ii Simo hupunguza hadhira
iii Simo huzuka na kutoweka
iv Baadhi ya simo huleta msamiati wenye matusi
v Simo huwa na chumvi nyingi au chuku nyingi hivyo haziaminiki katika jamii

5. Mwanafunzi na aoneshe kwa mifano dhahiri namna lugha ya kiswahili inavyoingiliana na lugha za kibantu( kikabila) huku akitoa mifano zaidi.(Alama 1.5@hoja , utangulizi 1)

- Mfanano katika kipengele cha msamiati mfano Kiswahili - Mtoto Kihehe -Uwana

-Mfanano katika kipengele cha tungo za kiswahili ( uwepo wa kiima na kiarifu) Mfano

Kiswahili Mama/ anakunywa maji

K A

Kinyakyusa Ujubha/ ukunywa amisi

K A

-Mfanano katika ngeli za nomino ( Upatanisho wa kisarufi)

Kiswahili Mtoto anacheza Watoto wanacheza

Kihehe Mwana akuhesigwa Vana vakwihesiga

-Mfanano katika vitenzi vya kiswahili( Mwanzo huanza na viambishi vya nafsi)

Kiswahili Njoo

Kinyakyusa Isaga

6. Mwanafunzi aoneshe ni sababu zipi zilifanya lahaja ya kiunguja iteuliwe katika usanifishaji (Alama 1.5@hoja)

(i)  Lahaja ya kiunguja ilikuwa imekwisha enea sehemu kubwa sana na kueleweka kartika nchi zilizokusudiwa  Mfano Zanzibar
(ii) Lafudhi ya kiunguja ilikuwa imekwisha tumika katika medani ya taaluma na kidini hasa Tanganyika, Uganda na Kenya
(iii) Lahaja ya kiunguja ilikuwa nyepesi zaidi kuliko lahaja zingine Mfano lahaja ya kimvita
(iv)  Lahaja ya kiunguja ilikuwa tayari kimsamiati ambapo uliweza kukidhi haja ya watumiaji wake
(v)  Lahaja ya kiunguja ilitumika sana katika biashara hasa pwani ya Afrika mashariki kulilo lahaja zingine
(vi) Lahaja ya kiunguja ilipewa hadhi kubwa zaidi kuanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu ya uongozi

7. Mwanafunzi anapaswa kuonesha idara zinzaosaidiana na BAKITA katika kutekeleza majukumu mbalimbali ( Alama 1.5@hoja utangulizi 1.5)
(i) Idara ya uhariri na uchapishaji
(ii) Idara ya lugha ya fasihi
(iii) Idara ya istalahi na kamusi
(iv)Idara ya uhusiano
(v)Idara ya tafsiri na ukalimani

8. Mwanafunzi na aonesha namna picha ya ganda la kitabu inavyotoa ujumbe kwa jamii( Alama 1.5@ utangulizi 1)

i. Picha ya watoto kupigana  inatoa ujumbe juu ya athari za kukosekana kwa upendo katika jamii kuwa chanzo cha mifarakano.
ii. Picha ya nguo chakavu walizovaa wanajamii inatoa ujumbe kuwa umasikini si suala mchekea katika jamii
iii. Picha ya wanajamii wakiwatazama wenzao wakipigana inaonesha ujumbe kuwa si vyema jamii ikakosa umoja na mshikamano kwani itashindwa kupata maendeleo
iv. Picha ya watu kugombana inatoa ujumbe kuwa jamii inapaswa kuwa na madilii

**SEHEMU  C( ALAMA 30) Mwanafunzi ajibu maswali mawili tu.**

9. Mwanafunzi na aoneshe kwa usahihi namna taashira/ jazanda/ taswira  zinavyoweza kuonesha maudhui mbalimbali kama zilivyotumiwa na waandishi.   CHA KUZINGATIA KITABU HUSIKA, MWANDISHI WAKE NA TAASHIRA HUSIKA ZINAZOBEBA MAUDHUI HUSIKA KWA JAMII.  Mfano Mwandishi ametumia taashira ya nahodha kuonesha umuhimu wa viongozi bora katika jamii.   ‘ nahodha’

10. Mwanafunzi aoneshe sababu zinazopelekea waandishi kutumia majina ya vitabu

    i. Kuvutia wasomaji
    ii. Kutoa ufupisho wa maudhui yaliyomo ndani ya kitabu
    iii. Husaidia na kuonesha falsafa ya mwandishi
    iv. Ni mbinu ya kifani inayoonesha uwezo na umakini wa mwandishi
    v. Husaidia kubaini wahusika wakuu kwa kubeba maudhui ya kitabu

Nb MWANAFUNZI AHUSIANISHE NA KITABU HUSIKA (Hoja tatu kwa kila tamthiliya)

11. Mwanafunzi na aoneshe namna nyimbo mbalimbali zilivyotumiwa na wahusika kwa lengo la kufikisha maudhui kwa jamii ( Mwanafunzi atumie riwaya katika kujibu swali)

**TAKADINI**

-Wimbo wa Rumbdizai kwa Sekai kuonesha suala la Kejeli (uk 2)

-Wimbo wa  Takadini kwa Mzee Chivero kuonesha suala la Upendo wa dhati wa --- Takadini kwa Mzee Chivero

-Wimbo Sekai kwa mtoto wake( Takadini) kuonesha suala la Ujasiri

-Wimbo wa watoto wa mtaani kwa Takadini kuonesha suala la Ubaguzi

**WATOTO WA MAMA N'TILIE**

- Wimbo wa mdundiko wakati wa asubuhi nje nyumbani kwa Mzee Lomolomo kuonesha suala uvivu na kutojituma kwa wanajamii

- Wimbo wa Mzee Lomolomo baada ya kunywa pombe na kulewa kuonesha suala la Ulevi

-Wimbo wa Kulwa baada ya kumiona mama na mtoto wake wanaenda matembezi kununua nguo kuonesha suala la Huzuni na masikitiko.

PIA MWANAFUNZI ANAWENZA KUTUMIA VITABU VINGINE VYA RIWAYA VIRIVYOORODHESHWA KWENYE MTIHANI WAKE.